**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Januari, 2026**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**


Anwani ya simu "**MKUU WA SHULE**"
Simu nambari: **0788462214**

SHULE YA SEK- RUANGWA WASICHANA
S.L.P. 93
RUANGWA


**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

**……………………………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA RUANGWA KIDATO CHA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2026.**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Napenda kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya wasichana Ruangwa **(shule ya bweni)** kwa mwaka wa masomo **2026** kama ilivyoainishwa hapo juu. Aidha Nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake, akumbuke kwamba hii ni bahati kubwa na ya pekee kwake.Shule ya Sekondari ya wasichana Ruangwa ipo kata ya Nachingwea Wilaya ya Ruangwa Mkoa wa Lindi. Shule ipo umbali wa mita mia tano (**500meter)** kutoka uwanja wa mpira wa Majaliwa (Majaliwa stadium) ukifika uwanjani (majaliwa stadium) fuata barabara inayoelekea kulia utakuwa umefika Shuleni bila shida.

Muhula wa masomo utaanza Januari, **2026** hivyo mwanao anatakiwa kuripoti shuleni siku shule itakapofunguliwa na hivyo unatakiwa kumleta mapema bila kuchelewa. Aidha ukichelewa kumleta mwanao atapoteza nafasi hii .Aidha unatakiwa kutekeleza maelekezo yafuatayo hapa chini.

## MAELEKEZO YA SARE ZA SHULE, VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA USAFI

### A. SARE ZA SHULE

- **i.** Sketi ndefu mbili (2) rangi ya draft ya kijani (dogdog), mshono ni rinda box mbele na nyuma. Kwa maelekezo Zaidi kuhusu sare, piga simu shuleni kupitia namba tajwa hapo juu.
- ii. Mashati mawili (2) meupe ya tetron mikono mirefu.
- iii. Jozi mbili za soksi nyupe zisizo na urembo/stocking.
- iv. T-shirt rangi ya KIJIVU yenye nembo ya shule kwa ajili ya sare ya shule ZITAPATIKANA SHULENI KWA TSH 15,000/=
- v. Sweta rangi ya kijivu
- vi. Kwa atakae vaa hijabu, avae sket ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu, nusu kanzu inayofunika makalio na hijabu kubwa kitambaa cha alua.
- vii. Viatu vya shule vyeusi vya ngozi, vyenye Kamba na visiwe na visigino.
- viii. Gauni 1 la kushindia rangi ya damu ya mzee (mshono wa solo hadi miguuni), na kwa anaevaa hijabu anatakiwa pia awe na hijabu ya damu ya mzee kwa ajili ya kushindia.
- ix. Sketi nyeusi 1 ndefu ya heshima na yenye marinda kwa ajili ya kushindia
- x. T-shirt 1 rangi ya bluu isiyo na maandishi
- xi. Raba nyeupe jozi moja,
- xii. Tracksuit yenye rangi ya bluu kwa ajili ya michezo.

B. **VIFAA MUHIMU VYA MWANAFUNZI**

i. Limu 1 ya karatasi kwa ajili ya majaribio ya kila wiki.
ii. Madaftari ya kaunta 10 saizi ya kati quare 2
iii. Begi la kubebea madaftari
iv. Mkebe mmoja wenye vifaa vyote vya kujifunzia
v. Kamusi ya kiingereza –kiswahili moja (English-kiswahili Dictionary)
vi. Rula ndefu ya futi moja nyeupe inayopituisha mwanga
vii. Madaftari za msomi 10 kwa ajili ya English course
viii. Sanduku la chuma lenye kufuri, kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake
ix. Godoro 1 jipya la sponji (futi 3 kwa futi 6), Zingatia vipimo vya godoro vilivyowekwa.
x. Chandarua (Neti) 1 ya rangi ya bluu
xi. Foronya 2 za rangi ya pinki na mto 1
xii. Shuka mbili za rangi ya pinki
xiii. Blanketi 1 rangi yeyote.

**C. VIFAA VYA USAFI NA AFYA**

i. AWE NA BIMA YA AFYA KUBWA, Kwa asiyekuwa nayo anatakiwa kuchangia kiasi Tsh. 50,400/= kupitia akaunti ya shule: **0150711059800 CRDB-RUANGWA GIRLS SECONDARY SCHOOL ( mzazi unasisitizwa kulipa hela ya bima kabla ya januari kwani Bima ya afya ni muhimu sana kwa afya na usalama wa mtoto wako)**
ii. Ndoo ndogo mbili mpya na kopo la kuogea
iii. Ndala za kuogea jozi 1
iv. Taulo moja/ kanga/ kitenge doti moja.
v. Mswaki na dawa ya meno
vi. Kitana cha nywele
vii. Mafuta ya mgando ya kupaka yasiyo na manukato wala kuchubua
viii. Jembe jipya moja lenye mpini na panga kwa ajili ya usafi wa mazingira
ix. Fagio ya chelewa yenye mpini mrefu
x. Fagio (Soft broom) moja,
xi. Brush kwa ajili ya kudekia chooni
xii. Skwiza moja kwa ajili ya kudekia chooni
xiii. Dawa ya chooni (Aro) lita 1
xiv. Sabuni ya maji lita 5
xiii. Aje na bakuli,
xiv. Sahani, kikombe, bakuli na kijiko kwa ajili ya chakula.
xv. Chupa kwa ajili ya kubebea maji ya kunywa

**D. viambatanisho muhimu vinavyopaswa kukabidhiwa shuleni na mwanafunzi pindi tu atakaporipoti**

i. Fomu ya kupimwa afya yake ambayo iotajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali ( fomu namba 1)
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai (fomu namba 3)
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia za shule, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ( Fomu namba 2)
iv. Picha za passport size 4 za ndugu wa karibu watakaokuja kumtembelea mtoto shuleni, na namba zao za simu.

NB:

- Kumbuka kumleta mwanao shuleni mapema iwezekanavyo na endapo hautamleta mtoto wako shuleni kwa wakati utachukuliwa hatua kali za kisheria ambapo ni pamoja na kupelekwa mahakamani kwa kosa la kutotimiza wajibu wako kama mzazi/mlezi.
- Kama zilivyo shule zote za bweni za serikali, shule ya sekondari Ruangwa Wasichana hutoa chakula safi na salama ambacho serikali imeelekeza kitolewe. Endapo unayo miiko ya kutokula baadhi ya vyakula, shule haitatoa huduma ya chakula Maalum (pekee) kwa kila mwanafunzi. Aidha, Pia shule haitoi kibali cha mwanafunzi kujipikia na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/kinywaji kutoka nje.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA RUANGWA**

**……………………………….**

**SHAREEN HATIB LUGONGO**

**MKUU WA SHULE.**

**0788462214**

**MAKAMU MKUU WA SHULE**

**0767818638**

**Nakala.**

- **DC-RUANGWA**
- **DED—RUANGWA**
- **AFISA ELIMU KATA**

**FOMU NAMBA 1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESEDENT OFFICE**
**REGION ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**RUANGWA DISTRIC COUNCEL**
**RUANGWA GIRLS SECONDERY SCHOOL**

**To the Medical Officer**
……………………………….
………………………………
…………………………………

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS**

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school students.

1. Pupil full name…………………………………………………………age……….
2. Blood…………………………………………………………….
3. Stool …………………………………………………………………..
4. T.B. Test ……………………………………………………………..
5. Syphilis Test ………………………………………………………………
6. Urine Examination…………………………………………………...
7. Eye Test ……………………………………………………………..
8. Chest Test…………………………………………………………………
9. Ears Test……………………………………………………………………..
10. Spleen…………………………………………………………………………
11. Abdomen ……………………………………………………………………
12. Pregnancy (for girls only) ……………………………………………………

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection, family diseases
etc…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

I certify that, the above pupil is suitable/unsuitable for secondary school students. If unsuitable give reasons:
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

Name of **Medical Officer**: …………………………………….. Signature
……………………………….
Date: …………………………………………

Official stamp………………………………………..

**FOMU NAMBA 2**

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA KANUNI ZA SHULE NA KUKUBALI PAMOJA NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA.**

Mmi………………………………………………….mzazi/mlezi wa………………………………..

Nimeyasoma kwa umakini sana maelekezo yaliyopo kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Ruangwa wasichana. Kwa hiari yangu nakubali mwanangu ajiunge na shule ya sekondari Ruangwa wasichana.

Niahaidi kuwa nitamsisitiza kuheshimu na kufuata taratibu, kanuni na sharia zote za shule. Endapo mwanagu atavunja sharia, kanuni na taratibu za shule basi achukliwe hatua kali stahiki kulingana na kosa atakalolifanya.

Saini ya mzazi/mlezi……………………………………………………….Tarehe…………………………

Saini ya mwanafunzi……………………………………………………….Tarehe……………………………

Saini ya mkuu wa shule…………………………………………………………Tarehe………………………

**FOMU NA 3.**

## MKATABA WA MWANAFUNZI KUHUSU KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi ………………………………………………………………………………….nimeyasoma kwa makini maelezo haya ya kujiunga na shule.kwa hiari yangu nakubaliana nayo.naahidi nitaheshimu sharia,kanuni na taratibu zote za shule na miongozo mbalimbali itakayo tolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.Aidha naahidi kuwa kwa vyovyote vile sitashiriki katika migomo,fujo na makossa ya jinai nikiwa shuleni au nje ya shule.

Endapo nitavunja sharia, kanuni, taratibu za shule, kushiriki katika migomo,fujo na kutenda makossa ya jinai basi nichukuliwe hatua stahiki kulinganana na kosa nitakalokuwa nimefanya.

Saini ya mwanafunzi…………………………………….tarehe…………………..

Saini ya mzazi/mlezi…………………………………… tarehe…………………..

Saini ya mkuu wa shule………………………………...  tarehe…………………..

**FOMU NA 4.**

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA RUANGWA**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara zenye dhamana ya Elimu nchini.

1.1 Mambo ya msingi ya kuzingatia ambayo pia utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni:-

a. Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima.
c. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa mwanafunzi wa shule hii.
e. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
f. Kuvaa sare ya shule wakati wote utakapotakiwa na kuzingatia ratiba ya shule.
g. Kwa kipindi chote ambacho mwanafunzi atakuwa shuleni, hataruhusiwa kuwa na nguo za nyumbani.

1.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule mara moja.

a. Wizi.
b. Uasherati na ushoga.
c. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
d. Kupigana na kupiga.
e. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
f. Kudharau bendera ya taifa.
g. kuolewa.
h. Kupata au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
i. Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki migomo au kuvunja amani na usalama wa shule au watu.
j. Kukataa adhabu kwa makusudi.
k. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.
l. Kukaidi maagizo ya shule.
m. Kumiliki na kutumia simu shuleni